

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) imezitaka Bodi za Wadhamini wa Taasisi ambazo hazijafanya marejesho ya wadhamini mpaka kufikia Mwezi Juni 2020 kufanya hivyo mara kabla ya hatua hazijachukuliwa kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kuzifuta Bodi hizo.



Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu Bi Emmy Hudson

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari, RITA imetoa Orodha ya Bodi za Wadhamini wa Taasisi 100 ambazo zina malimbikizo ya marejesho mpaka kufikia mwezi Juni 2020 ambazo miongoni mwao ni Bodi za Vyama vya Siasa na Taasisi za Dini na Taasisi za Kijamii.

RITA inaendelea na zoezi la uhakiki wa kina wa Bodi za taasisi zote zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wadhamini Sura ya 318, lengo likiwa kufahamu hali ya kila taasisi kama zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na katiba za taasisi husika. Wakati Uhakiki ukiendelea Bodi za taasisi hizo zinatakiwa kuwasiliana na Wakala ili kuhakiki taarifa zao na kwa upande wetu RITA tayari tumeanza kuzitembelea Ofisi za taasisi hizo.

Muunganisho wa Wadhamini ni utaratibu unaohusisha usajili wa wadhamini ambao huwezesha wadhamini waliounganishwa (trustees incorporation) kuwa na utu wa kisheria, kuweza kushitaki au kushitakiwa kwa jina lake, kumiliki na kuuza mali na kuingia katika mikataba kwa niaba ya taasisi hizo. Mfumo huu wa Muunganisho wa Wadhamini unaongozwa na Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 Toleo la 2002. (*The Trustees' Incorporation Act, CAP 318 R.E.2002*).

RITA ni taasisi Serikali yenye dhamana ya kusajili na kusimamia utendaji kazi wa Bodi za Wadhamini wa Taasisi na tunazikumbusha kwamba zina dhamana kubwa ya kusimamia mali za Taasisi hizo kwa uadilifu na weledi.

Ijulikane kwamba wadhamini wa Taasisi wanawajibika kisheria kama mdhamini mmoja mmoja au kwa pamoja endapo uzembe au ubhadrifu utajitokeza katika utendaji wake wa kazi. Tunatoa rai kwa Bodi za Wadhamini kuzingatia Sheria ya Usajili wa Wadhamini ikiwemo kutoa Taarifa mara mabadiliko yanapotokea na kuleta Marejesho ya kila Mwaka.

Kwa mujibu wa Sheria, Bodi ambazo hazitekelezi majukumu yake kikamilifu zinatakiwa kufutwa katika Daftari la Msimamizi Mkuu wa Wadhamini na zitapaswa kurejesha mara moja hati za usajili (*certificate of Incorporation*) kwa Kabidhi Wasii Mkuu kulingana na kifungu cha 23(4) cha Sheria ya Usajili wa Wadhamini. Mali za Taasisi/Asasi hizo zinawezwa kuwekwa chini ya usimamizi wa Mdhamini wa Umma (Ofisi ya RITA) endapo kutakuwa na ombwe la Wadhamini mpaka hapo utaratibu mwingine utakapotolewa.